



## SALA KWA YESU MWABUDIWA



Ee Yesu mnyenyekevu, unayeabudiwa na uliye ndani ya Sakramenti Takatifu ya Upendo Wako Mkuu. Nikiwa hapa mbele ya kiti chako kitukufu cha enzi kilichofichika, ninaweka roho yangu na mwili wangu wote mbele yako. Kutokana na hali yangu ya unyonge na dhambi zangu, ninakuomba upokee sala zangu duni na matendo yangu ya malipizi ya dhambi na ya kukuabudu, ili kutuliza kiu yako kwa roho zetu, na utupatie msamaha kamili kwa ajili ya wingi wa dhambi za kufuru, kukosa shukrani na matusi ambayo unapokea daima kutoka kwetu sisi wenye dhambi.

Ni huruma yako ya milele kwa wanadamu ambayo ilikufanya ujitolee na kujishusha hali ili uweze kukaa nasi kwa upendo katika altare na tubenakulo ulimwenguni pote.

Ee Yesu, kutokana na Roho, Mwili na Umungu wako, ambayo vipo ndani ya Ekaristi Takatifu, pokea majonzi ya roho yangu ili roho unazozithamini sana zisipoteze kabisa uhai wao wa milele: (taja majina ya wale unaotaka kuwaombea).

Nyakati zote hadi milele ni mali yako. Kwa hiyo, tunajitoa kikamilifu na kujiweka kwa imani chini ya ulinzi wako wa upendo, wakati huu tukiwa hai na tutakapokufa. Amina.

Sista Anna Ali apokea sala hii kutoka kwa Bwana Yesu mwezi wa Agosti, mwaka wa 1987.

## SALA YA SAA ZETU ZA MWISHO

Ee Yesu, unayeishi daima na mwenye huruma. Kwa moyo mnyenyekevu ninajongea kwako ili nikutolee hali ya saa zetu za mwisho za uhai. Saa ile, Ee Yesu, wakati ambao hatutaweza tena kutumia maumbile yetu, na roho zetu zitakuwa na majonzi zikipambana na kuhuzunishwa na kifo, wakati ule ambao roho zetu zitabidi kujitenga na miili yetu ya kibinadamu na kutoka duniani, Yesu utuhurumie. Utusamehe na kupokea hali zetu za mwisho wakati wa kifo. Hakika Wewe ndiye uliyekuja ili tupate uzima kamili. Amina.

Sista Anna Ali apokea sala hii kutoka kwa Bwana Yesu tarehe 1, Aprili, mwaka wa 1991.